



www.aidboxcommunity.co.uk

AidBoxConnections

Kupunguza kutengwa, kujenga urafiki na jamii

Huduma hii ni ya: - Watu waliopoteza makao (wakimbizi na watafuta stara) na ambao sasa wanaishi Bristol, wangependa kukutana na rafiki na kujihisi kuwa ni sehemu ya jamii.

Jinsi inavyofanya kazi: Tutakuambatanisha na 'Rafiki wa Connection', mtu anayejua Bristol na mwenye ari ya kupata rafiki mpya. Atakupigia simu mara mbili kwa wiki kwenye wakati ulio mwafaka kwa nyote wawili. Baada ya wiki 12, unaweza kuchagua:

1. Kuendeleza urafiki wako unaokua bila kuihusisha ABC
2. Kukomesha mawasiliano
3. Kujuana na mtu mwingine

Tutaendelea kuwasiliana na wewe kwenye wiki 12 na tutakuwa tunapatikana uwasiliane na sisi wakati wowote ukiwa na matatizo yoyote.

Rafiki wa Connection yuko hapo kwa ajili ya urafiki na ili kupunguza hisia za kutengwa au matatizo ya kutoa ushauri. Marafiki wetu wote wa Connection wamepokea mafunzo kuhusu huduma zinazopatikana huko Bristol zinazosaidia wakimbizi na watafuta stara, ili waweze kukusaidia utafute usaidizi unaoweza kuuhitaji. Pia wanasimamiwa kwa karibu ili tuweze kuhakikisha usalama wa kila mtu.

Mawasiliano yote yatakuwa kwa simu, WhatsApp, simu ya video -**KATU** hamtokutana ana kwa ana kwenye mpango wa wiki 12.

Imogen na Naomi ni waratibu wa Aid Box Connections na unaweza kuwasiliana nao ikiwa una wasiwasi au matatizo yoyote kuhusiana na huduma.

- Imogen 07378 663110 imogen@aidboxcommunity.co.uk
- Naomi 07378684891 naomi@aidboxcommunity.co.uk

Taarifa ya Faragha

Maelezo tutakayoshiriki ni jina na nambari yako ya simu tu isipokuwa ikiwa tuna wasiwasi kuhusu usalama wako au wa mtu mwingine. Ni juu yako maelezo gani mengine unayotaka kuyashiriki na Rafiki wako wa Connection.